



# HABARI.

'Manyara Home of elephant''

manyara_rs

www.manyara.go.tz

## MAONESHO YA SIKUKUU YA NANE NANE KWA MIKOA YA KANDA YA KASKAZINI.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mh Queen Sendiga amewaongoza maelfu ya wakazi wa Mkoa wa Arusha katika kilele cha maadhimisho ya sikukuu ya wakulima.



Tarehe 8. 8. 2023 ni sikukuu ya ya wakulima inayofanyika kila mwaka. Sikukuu hiyo kwa mwaka 2023 imefanyika kikanda ikijumuisha mikoa ya Arusha Kilimanjaro pamoja na Mkoa wa Manyara mikoa ambayo inakamilisha ujumla wa mikoa ya ukanda wakaskazini.

Kilele cha maadhimisho ya sikukuu ya wakulima kwa mwaka 2023 kimefanyika kikanda katika Mkoa wa Arusha kwenye viwaja vya Themi jijini Arusha.




Ambapo Mh.Queen Sendiga akiwa ndiye mgeni rasimi watukio hilo kubwa, sambambana hilo Mkuu huyo wa Mkoa wa Manyara ametembelea mabanda ya maonyesho pamoja na kuhutubia umma uliyojitokeza.

Amewataka wadau na wananchi kutumia fursa zilizopo katika kilimo cha umwagiliaji ilikukabiliana na mabadiriko ya tabia ya nchi. katika tukio hilo Mkuu wa Mkoa wa Manyara ametoa rai kwa wataalamu na maafisa wa kilimo kuyafikia makundi ya wanawake vijana na wananchi kwa ujumla ilikuwaongeza elimu na ufanisi katika shughuli za kilimo na ufugaji.

Aidha ameeleza kuwa Serikali imeendeleakutekeleza miradi ya umwagiliaji kwenye ukanda wa mikoa ya kaskazini yenye thamani ya jumla ya Bilioni 47.64. vile vile ameeleza mpango wa Serikali kujenga visima 150 kwa kila Halmashauri ilikuleta mapinduzi katika Sekta ya umwagiliaji.



Pia Mh.Queen Sendiga ameongeza siku mbili zaidi kwa maonyesho hayo kuendelea katika viwanja hivyo baada ya kuridhishwa na maonyesho kwa wakulima, wananchi na wanafunzi waliyojitokeza kujifunza kupitia maonesho hayo.





# HABARI .

'Manyara Home of elephant''

manyara_rs

www.manyara.go.tz

# MAFUNZO YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2020 -2050 MKOA WA MANYARA

Wizara ya fedha na mipango tarehe 18. julai. 2023 imeendesha mafunzo mafupi kuhusu Dira ya maendeleo ya Taifa 2050 katika Mkoa wa Manyara.

Ambapo kaulimbiu ya mafunzo hayo ni ''shiriki katika kuijenga Tanzania uitakayo'' mafunzo hayo yamefunguliwa na Mh.Queen Sendiga Mkuu wa Mkoa wa Manyara.




Katika ufunguzi wa mafunzo hayo Mh.Queen Sendiga amewaeleza washiriki katika mafunzo hayo lengo la mafunzo-hayo nikupata uelewa wakutosha kuhusiana na dira ya maendeleo 2050, Aidha amewambia washiriki Dira hiyo inagusa maeneo yote katika Taifa hivyo kuna ula zima wa kila mwananchi kuwa na uwelewa huo.

Amewaambia washiriki kuwa mafunzo ni pango mahususi katika kuhamasisha wa Tanzania wote na kuweka wepesi wakuweza kutumia mawazo ya kila mwaanchi, Amewahakikishia wataalamu waliyoendesha mafunzo hayo kuwa uhamasishaji huwo kwa Mkoa wa Manyara utashuka hadi katika ngazi za wilaya na vitongoji

Sambamba na hayo Mkuu wa Mkoa - amewataka wakurugenzi katika Halmashauri zote za Mkoa wa Manyara kupeleka uhamasishaji huwo katika ngazi za kata, ikiwa nikuwapatia taarifa za mafunzo hayo watendaji wa kata na wenye viti wa mitaaa ili kila mtanzania awe na uwelewa wakutosha kuhusu Dira ya maen - deleo ya Taifa 2050.

Aidha mjumbe wa kamati ya maandalizi ya mafunzo hayo (SoSthenes Kewe) - kutoka wizara ya fedha na mipango ameeleza kuwa kwasasa inatumika Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Ambapo Dira hiyo ya 2025 ilikuwa nikuhakikisha Taifa linaingia katika uchumi - wa kati ambao unachagizwa na kuboresha hali ya maisha kwa mtanzania kujenga utawala bora kujenga uchumi imara na shindani.

Mjumbe huyo ameeleza umuhimu wa kuleta mafunzo hayo katika ngazi ya Mk oa ikiwa niutekelezaji wa Dira huku kio ngozi mkuu wa Dira hiyo ya mwaka 2050 akiwa ni Mh.Rais SamiaSuluhu Hasani huku wenye dhamana wakiwa ni viongozi wa Mkoa.



# HABARI..

‘Manyara Home of elephant’’

manyara_rs

www.manyara.go.tz

# TUVUNJE UKIMYA

## KIKAO CHA MRADI WA UTAFITI WA SOKO LA SODO....

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa kikao hicho Katibu Tawala Mkoa wa Manyara ame shukuru shirika la OIKOS na wizara ya Afya kwakuleta mradi huwo wa utafiti kwaku saidia suala la sodo kwa mabinti wakike mashuleni Pia ameelezakuwa kufanikiwa kwa mradi huwo - kutasaidia kuongeza mahudhu rio shuleni kwa - mabinti wengi.



Katibu Tawala Mh.Karolina Mthapula akihutubia wadau katika kikao kilichoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la OIKOS

Amewataka watu kuwapa ushirikiano waku tosha shirika hilo la OIKOS ushirikiano ambao utaweza kurahisisha ufanikishaji wa mradi huwo.

Nukuu ya maneno ya Mh Karolina Mthapula (Katibu Tawala Mkoa wa Manyara).
Aidha ameeleza ukosekanaji wa sodo unaweza kukatisha ndoto za mambinti wengi,
Pia ameeleza kuwa kufanikiwa kwa mradi huwo kutasaidia kuongeza mahudhurio shuleni kwa mabinti wengi.

## KATIBU TAWALA ASISITIZA HEDHI SALAMA

suala la hedhi salama ni suala la kitaifa ambalo kila mtu kwenye-jamii kulichukulia katika uzito, ame-eleza kuwa ufanikishaji wa mradi - huwo utakuwa umesaidi Taifa.

Afisa Afya Mkuu wizara ya Afya meeleza umuhimu wa Afya kwa akina mama wa badae ikiwa ni kuongeza uwelewa kwa jamii, ambapo ameeleza juu ya kau limbiu ya wizara
‘’TUVUNJE UKIMYA’’
ikiwa ni uchochezi mkubwa wa kila mtu kwenye jamii awe na uwelewa nakupaza sauti yake katika kueli misha umma juu ya hedhi salama.

# HABARI.

'Manyara Home of elephant''

manyara_rs

www.manyara.go.tz

## ZIARA YA NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU AJIRA VIJANA NA WALEMAVU

Ni ziara ya Naibu waziri ofisi ya waziri Mkuu vijana ajira na watu wenye ulemavu Mh. Patriobasi Katambi amefanya ziara, Mkoa wa Manyara 11/8/2023, akiambatana na Naibu Katibu Mkuu ofisi ya Waziri Mkuu

Ambapo amepokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mh Queen Sendiga. Ziara hiyo yenye lengo la ukaguzi wa maandalizi ya shughuli za sherehe kilele cha mbio za mwenge zinazotaraji wa kufanyika Mkoa wa Manyara mwezi Oktoba 14, 2023.



Sambamba na kupokewa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara. Amepokea taarifa fupi kuhusu maandalizi yanayoendelea kufanyika, ikiwa nipamoja na upandaji wa nyasi ambao umekwisha fanyika katika uwanja unao andaliwa kwajili ya kilele cha mbio hizo.

Pia ameeleza juu ya kupatiwa vifaa kutoka kwa wadau nakupewa vijana wa JKT kwajili yakufanya maandalizi yanayoendana na muda uliyowekwa kwajili yaukamilishaji wa uwanja.

Hata hivyo Mh Queen Sendiga amemueleza Naibu Waziri kuwa kunachangamoto katika ujenzi wa kiwanja hicho cha kwaraa,changamoto kubwa ikiwa ni uhaba wa fedha ameishukuru ofisi ya waziri mkuu kwakutoa Milioni 600 kwajili ya maandalizi ya uwanja huo.

Mh. mkuu wa Mkoa ameeleza upandaji wa nyasi katika uwanja wa kwaraa umefanyika kwa msaada wa shirikisho la mpira wa miguu nchini TFF.

Ameshukuru ofisiya Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo inashirikiana na ofisi yake ya Mkoa kwa ukaribu ilikuweza






# HABARI MANYARA.

'Manyara Home of elephant''

manyara_rs

www.manyara.go.tz

## ZIARA YA MAKAMU MWENYEKITI

### WA CHAMA CHA MAPINDUZI TANZANIA BARA MH. ABRAHAMANI KINANA MKOA WA MANYARA

Julai 24.2023 saa nne asubuhi katika eneo la kijiji cha Bonga nje kidogo ya mji wa Babati Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mh. Queen Sendiga.

Akiambatana na katibu Tawala Mkoa wa Manyara (Mh.Karolina Mthapula) na viongozi wa Ccm Mkoa wa Manyara akiwemo mwenye kiti wa Ccm Mkoa na kamati nzima ya siasa Mkoa.



Ziara hiyo ya Comrade Abrahamani Kinana Makamu Mwenyekiti wa chama cha mapinduzi Tanzania bara nikwajili ya kuimarisha chama cha mapinduzi katika Mkoa wa Manyara, Amepokelewa na wananchi wa Bonga kwa furaha huku wananchi wengi wakijitokeza katika eneo hilo.

Mala baada ya mapokezi katika eneo la kijiji cha Bonga Comrade Kinana. Amefanya kikao katika jengo la Ccm Mkoa na wakuu wote wawilaya na wakurugenzi wa Halmashauri zote katika Mkoa wa Manyara katika -kikao hicho Comrade kinana amepokea taarifa fupi kutoka kwa katibu wa Ccm Mkoa wa Manyara.



Aidha katibu wa Ccm Mkoa katika kuwasilisha kwake taarifa hiyo fupi ameshukuru chama cha mapinduzi kuendelea kutekeleza iraniya chama kwakuweza kuleta miradi mingi ya maendeleo katika Mkoa wa Manyara.

Pia amemshukuru Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Mh.Samia Sul-uhu Hasani kwakutoa fedha nyingi ka-tika Mkoa wa Manyara katika maeneo mbalimbali ikiwemo elimu,Afya na uje nzi wa shule kila wilaya na vituo vya Afya katika ngazi ya kata na wilaya.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara katika kuw asilisha taarifa ya Serikali, Amemshuku ru Mh Rais Samia Suluhu Hasani kw akutoa fedha za utekelezaji wa miradi, Ameleeza kuwa hali ya usalama katika Mkoa wa Manyara ni nzuri na hakuna shida yoyote pia ameshukuru kwa mab-oresho ya miundo mbinu ya elimu kwa jinsi ilivyofanikiwa katika Mkoa wa Man yara.

Katika kuwashilisha taarifa hivyo Mh - Queen Sendiga amemueleza makamu mwenyekiti Tanzania bara Comrade Ab rahamani kinana kuwa Mkoa wa Manya ra, katika makusanyo yake ya fedha ka tika ngazi ya Mkoa umefanikiwa kukus anya Bilioni kumi na tisa hiyo nikutoka na na ripoti ya mkaguzi Mkuu wa Serik ali ya mwaka wa fedha uliyopita 2022-2023 ikiwa ni ongezeko zaidi ya maku sanyo yaliyopita.

Sambamba na hayo Mh Queen Sendiga amemuelezea Comrade kinana kuwa kunachangamoto pamoja nakuwa na mafaniko hayo katika Mkoa,

Miongoni mwa changamoto hizo ni pam oja na upungufu wa waalimu kwa baad hiya maeneo katika Mkoa wa Manyara changamoto ya uhaba wa wataalamu wa Afya katika Mkoa wa Manyara chan-gamoto za migogoro ya Aridhi.

Baada ya mazungumzo hayo Mh Queen Sendiga amemkabidhi Comr ade Abrahamani kinana ripoti ya Se rikali huku tukio hilo likishuhudiwa na wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Manyara.

Pamoja na tukio hilo Comrade kinana amefanya kikao na wanachama cha mapinduzi Mkoa wa Manyara katika ukumbi wa mikutano uliyoko katika je ngo la Ccm Mkoa wa Manyara, Amew apongeza wanachama wa Ccm Mkoa wa Manyara kwakuimarisha chama k atika ngazi zote wilaya na mpaka kwe nye kata na vijiji.

Amewakumbusha majukumu yao - wakuu wa wilaya kuwa wao ni nguzo kati ya chama na Serikali ameeleza pia kila zuri ambalo wanachama wa Ccm Mkoa wa Manyara wameliona au kushuhudia limetokana na sera nzuri ya chama cha mapinduzi.

Katika ziara yake Comrade kinana ametembelea eneo la Daleda kati kata ya Ayalagaya ambapo aliamba tana na Mkuu wa Mkoa na kamati nz ima ya chama cha mapinzudi Mkoa wa Manyara

Mbunge wa Babati vijijini ambae nd-iye mwenyeji wa eneo hilo Mh.Daniel Siro amempongeza Mh.Rais Samia Suluhu Hasani kwa utekelezaji mzuri wa irani ya chama cha mapinduzi.

Sambamba na hayo Mbuge huyo am ewatoa hofu kuhusu tatizo la maji k-wa wananchi wa kata ya Ayalagaya kwakuweza kufanikisha mradi mkub wa wa maji ndani ya muda mfupi kati ka kata hiyo.

Ameeleza juu ya kufanikisha ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Babati vijijini lak ini pia upokeaji wa fedha za Tasaf kwa kaya zisizo jiweza kiuchumi ufanikishaji wa ujenzi wa madarasa katika kata hiyo.

Aidha Comrade Abrahamani kinana ka ika kuongea na wananchi wa kata ya Ay-alagaya amemshukuru Mbunge Daniel - Siro kwa kazi nzuri anayoifanya,

Amezungumzia utekelezaji wa mradi wa maji kupitia mdau aliyejitokeza katika ka ta ya Ayalagaya. Amemuhakikishia mda u huyo kufanya kazi kwa uhuru na kuon geza miradi mingine katika Sekta ya eli-mu na Afya amezungumzia juu ya chang amoto ya wawekezaji kuingilia maene-o ya wakulima katika kata ya Ayalagaya-kuwaachia maeneo ilikuepuka migorogo ro kati ya wananchi na wawekezaji.